EAFPAM
PL8704
.B29
Z2

ZAKA LA DAMU

SHERIA YA KUNAKILI,
©BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA,
DAR ES SALAAM, TANZANIA.

Mhariri: Ndugu S. N. C. F. Masoza
Picha (Jalada) Ndugu G. O. Diaz
Wasanii: Ndugu L. M. Thonya/R. M. Haule

Chapa ya Kwanza 1976
Chapa ya Pili 1982

KIMEPIGWA CHAPA NA PRINTPAK (T) LTD.
S.L.P. 9240, DAR ES SALAAM

YALIYOMO

Ukurasa

1. **MSIBA** —
Mwandishi: Joseph Mkomagu.....1 — 22

2. **SIKUDHANI** —
Mwandishi: Mary M. Salimu.....23 — 79

3. **ZAKA LA DAMU** —
Mwandishi: Harrison Mwakyembe.....80 — 108

UNIV. OF DAR ES SALAAM LIBRARY

Mtu aliyeingia, hakuzoea kuikuta chai mezani saa kama zile. Siku hiyo basi, yalikuwa maajabu. Aliichukua chupa pamoja na kikombe akaenda navyo chumbani kwake. Magomvi ya dhamira yalianza: "Kunywa basi!" "Kunywa na wewe." "Siyo kawaida yangu. Lakini ..... Hapana siyo heshima." .....

Kwa upesi sana macho yake yaligeuka rangi ya njano. Kila alipotazama aliona giza tupu. Kichwa kikamuwanga sana; moyo ukachukua mapigo ya nguvu na ya haraka sana. Tumbo likachemka. Ndipo alipotambua kasoro. Hapo akatoka nje haraka sana. Akachukua mayai mawili ya kuku. Akayavunja haraka katika kikombe, akakoroga pamoja na chumvi, kisha akayanywa. Mara moja akatapika vyote. Yu mzima sasa, alirudi kitandani na kujitupa kimya kana kwamba hapana baya lolote lililotokea.

Usiku wa manane, mwanamke aliamka na kunyemelea chumbani kwa Ndatu ili akahakikishe. Loo! Anakoroma kwa amani. Yu mzima mwenye afya. "Lakini chai je?" Mara akashtuka na kujisemea, "Mama wee! Nalimsikia akitapika!" Lahaula! Alichodhamiria kimemkimbia; nacho kiko nje sasa. Kwa hofu kubwa alirudi chumbani kwake akafunga baadhi tu ya mizigo. Kisha aliandika barua fupi akaitupa mezani, halafu akatokomea gizani.

Asubuhi, Ndatu aliamka mzima kabisa. Alipoiona barua mezani, aliifungua na kuisoma:

Mpenzi Ndatu,

Nasikitika kwamba mapenzi yetu yamekoma. Tangu zamani sikupendezwa na mawazo yako ya kujihusisha na Wafakiri. Baada ya kifo cha baba, umewagawanyia Wafakiri mali yake yote. Ulifikiri tutachumaje mali kama siyo kwa kuwatumia Wafakiri? Kama marehemu baba angalikuwa mjinga kama wewe, hapana shaka asingalikuwa na mali nyingi. Sina haja ya kuishi na mtu mwenye mawazo ya umasikini.

Pia ni ajabu sana kuona kwamba u mhusika mkuu katika kifo cha baba ambaye alikukirimu kwa muda mrefu sana. Kumwua ndiyo shukrani yako. Rafiki yako Kabamba amenieleza yote. Niliamua kukuua leo. Lakini ujanja wako! Nimeamua sasa kurudi kwetu!

Ni mimi niliyekupenda,
Maua.

Kama samaki katika nyavu za mvuvi, jambo ambalo Ndatu alikuwa akilitafuta lilijileta mikononi mwake. Kukatika kwa kamba ilikuwa furaha kubwa sana kwake.

Baada ya kuisoma barua ya Maua, Ndatu alikaa pale ukumbini huku akifurahi kwa kuwa jaribu la kumuua halikufanikiwa. Tena furaha ilizidishwa na kutoweka kwa Maua katika nchi ya Fakiri. Tangu kuwasili kwake katika Fakiri, Ndatu alikuwa akijaribu kwa nguvu zake zote kuzing'olea mbali ndago, na kuziondoa katika jamii ya miche ya mpunga. Ndago lakini ni nyasi za ajabu sana. Kila mara Ndatu alipozing'oa haukupita muda mrefu kabla nyingine hazijaota. Hata hivyo Ndatu hakukata tamaa, mwaka hata mwaka aliendelea na bidii ile ile.

.....

Wakati Maua akitafuta kulipiza kisasi, Kabamba alikuwa mbali sana na kijiji cha Kaninga. Midomoni mwa Wafakiri wengi, Kabamba sasa alikuwa mchungu mno, ingawa yeye mwenyewe hakujua. Ndatu kadhalika aliathiriwa na uchungu wa Kabamba. Mara kwa mara Ndatu alikuwa akimweleza Kabamba ubaya wa kutaka makuu. Ubaya wa mtu kujitazama akatosheka, kwa kuwa yeye pekee ameshiba. Ni shida kubwa basi kwa mtu wa aina hii kumtazama jirani yake. Njaa ya mwenzake haina uhusiano na maisha yake. La muhimu kwake ni yeye binafsi kushiba.

Tangu Kabamba achaguliwe na Ndatu, amepanda mlima mrefu sana. Watu wote walikuwa chini ya miguu yake. Wanawake kwake walikuwa nguo. Yeye mwenyewe ni malaika ingawa hakuwa. Alikuwa Mtukufu wa kutukuzwa. Ajabu hakutukuka! Ili kuwateka watu alijionyesha asivyo; hali ukweli ulifungiwa kama moyo wa mtu ulivyo mwilini. Awapo simba hujitoa kama paka, na awapo nyoka hutokea kuwa mjusi. Lakini ni binadamu wangapi wasiokuwa na vichwa vikamilifu? Mafichuo ni kufichua kilichofichwa.

.....

Usiku ule wakati akirudi Kaninga, Kabamba alikuwa akihema sana; labda alikuwa amekimbia sana. Giza lilikuwa nene la